TANGAZO LA SERIKALI NA. 319 la tarehe 26/4/2024

SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI.
(SHERIA NA. 1 YA MWAKA 2024)

# NOTISI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 49(2))*

UCHAGUZI WA KITAIFA (TANGAZO LA NAFASI YA WAZI YA KITI CHA MBUNGE (JIMBO LA KWAHANI), 2024

Sheria Na. 1 ya Mwaka 2024

**KWA KUWA,** Kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kinampa Mamlaka Spika wa Bunge la Tanzania kutangaza nafasi ya Ubunge pale Mbunge anapojiuzulu, anapofariki dunia au anapojiuzulu kwa sababu nyingine tofauti na zilizoainishwa chini ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani chini ya Kifungu cha 142 cha Sheria hiyo.

**NA KWA KUWA,** kufuatia kifo cha **MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL** aliyekuwa Mbunge, Jimbo la Kwahani aliyedhaminiwa na Chama Cha Mapinduzi **(CCM)** alifariki dunia tarehe 08 Aprili, 2024

Sheria Na. 1 ya Mwaka 2024

**KWA HIYO SASA,** MIMI DKT. TULIA ACKSON, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa madaraka aliyopewa Spika chini ya Kifungu cha

49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani nautaarifu Umma kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Uchaguzi wa Kitaifa (Tamko la kuwa wazi kwa Nafasi ya Kiti cha Mbunge wa Jimbo la Kwahani) 2024

Tangazo

2. Kiti cha Ubunge wa Jimbo la Kwahani Zanzibar kinatangazwa kuwa kipo wazi.

Dodoma
16 Aprili, 2024

DKT. TULIA ACKSON (MB)
*Spika*